



Muhtasari kwa Waandishi wa Habari: Siku ya Kimataifa ya Mshikamano na Watu wa Palestina 2020

Suala la Palestina ni miongoni mwa masuala ya muda mrefu ambayo hajjasuluhishwa katika ajenda ya Umoja wa Mataifa. Wakati Azimio la Baraza Kuu 181 (ii) la 1947 lilitaka kuundwa kwa mataifa mawili, watu wa Palestina bado hawajaweza kupata nchi yao na miaka 70 baadaye, kuna zaidi ya wakimbizi wa Kipalestina milioni 5 wanaoishi nje ya nchi yao, wakisubiri kurejea. Maazimio mfululizo ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa na Baraza Kuu yametaka kukomeshwa kwa uvamizi wa ardhi ya Wapalestina tangu 1967 na kuunga mkono kuundwa kwa Dola ya Palestina kwenye mipaka ya kabla ya 1967, na Yerusalemu Mashariki ikiwa mji wake mkuu. Maazimio ya Umoja wa Mataifa - Azimio la hivi karibuni la Baraza la Usalama 2334 la 2016 - pia yameona kuwa haramu makazi ya Israeli yaliyojengwa kwenye ardhi ya Palestina inayokaliwa kwa mabavu.

Jumuiya ya kimataifa inaendelea kuwa thabiti katika ahadi yake ya kuhakikisha maisha ya uhuru na heshima kwa watu wa Palestina. Tangu 1977, Umoja wa Mataifa umeashiria kupitishwa kwa azimio la Baraza Kuu 181 (ii), kama Siku ya Kimataifa ya Mshikamano na Watu wa Palestina kwa kuwa na mikutano na hafla maalum katika Makao Makuu ya UN huko New York, na katika ofisi za UN huko Vienna, Geneva, Nairobi na kwingineko.

Mwaka huu, Siku ya Kimataifa ya Mshikamano na Watu wa Palestina itaadhimishwa tarehe 1 Desemba kwa mikutano maalum. Katika makao makuu ya Umoja wa Mataifa huko New York, Kamati ya Utekelezaji wa Haki zisizoweza kuepukika za Watu wa Palestina, chombo cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa linalotangaza haki ya watu wa Palestina ya kujitawala na kujitegemea, itawakutanisha maafisa wa ngazi ya juu wa nchi wanachama, Katibu Mkuu, mashirika ya serikali na wawakilishi wa asasi za kiraia ambao wanatarajiwa kutoa maelezo kuhusu suala la Palestina na kuhudhuria uzinduzi rasmi wa maonesho yanayoangazia Ukuta uliojengwa katika Taifa la Palestina linalokaliwa kwa mabavu, ambalo limetajwa kuwa haramu na Mahakama ya Haki ya Kimataifa katika Maoni yake ya Ushauri ya 9 Julai 2004.

Maonesho yanaangazia haya kupitia maneno ya watetezi na watu mbalimbali wenye haiba ya umma, na kupitia picha kutoka kwa wasanii na wanaharakati wa haki za binadamu ambao wametumia ukuta huo kama turubai la kuchorea kuelezea mshikamano wao na watu wa Palestina. Matukio hayo yatarushwa mubashara kupitia UN Web TV [<http://webtv.un.org/>] na maonesho yatatapikana kwenye tovuti ya Umoja wa Mataifa.

Shughuli pia zitaandaliwa kwenye hafla hiyo na mashirika ya serikali na AZAKI kwa kushirikiana na vituo vya habari vya Umoja wa Mataifa kote ulimwenguni. Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa litakutana mwaka huu kwa mjadala wake wa kila mwaka juu ya suala la Palestina mnamo tarehe 2 Desemba, ambapo linatarajiwa kupitisha kwa idadi kubwa azimio linaloelezea vigezo ya suluhisho la haki kwa suala hili lililobaki.

Tufuate kwenye mitandao ya kijamii:



<http://www.facebook.com/UN.palestinianrights>



<http://www.twitter.com/UNISPAL>



<http://www.youtube.com/UNpalestinianrights>



<https://www.instagram.com/unispal/>